TANGAZO LA SERIKALI NA. 616 la tarehe 25/8/ 2023

SHERIA YA HIFADHI ZA TAIFA
(SURA YA 282)

---

**TAMKO**

---

*(Limetolewa chini ya kifungu cha 4)*

TAMKO LA KUFUTA HIFADHI YA TAIFA KIGOSI LA MWAKA 2023

KWA KUWA, kifungu cha 4 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa kinampa Rais mamlaka ya kufuta eneo lolote lililotangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa baada ya kupata idhini ya Bunge;

NA KWA KUWA, idhini ya Bunge imetolewa kupitia Azimio la Bunge la Kuridhia Kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa Kigosi, Azimio Na. 03/2023 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameridhika kwamba kuna sababu za kutosha kumwezesha kutekeleza mamlaka hayo katika Hifadhi ya Taifa Kigosi;

HIVYO, katika kutekeleza mamlaka aliyopewa Rais chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa na kwa Idhini ya Bunge iliyotolewa tarehe 27 Juni, 2023, Mimi, SAMIA SULUHU HASSAN, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania natamka ifuatavyo:

Jina

1. Tamko hili litajulikana kama Tamko la Kufuta Hifadhi ya Taifa Kigosi la Mwaka 2023.

Kufutwa kwa Hifadhi ya Taifa

2. Hifadhi ya Taifa Kigosi inafutwa.

Kufutwa kwa TS Na. 924 la mwaka 2019

3. Tamko la Kutangaza Hifadhi ya Taifa ya Kigosi linafutwa.

Imetolewa kwa sahihi yangu na lakiri ya Umma hapa Dodoma leo tarehe 6 Mwezi Agosti 2023.

Dodoma,
6 Agosti, 2023

SAMIA SULUHU HASSAN
*Rais*